


# **Umoja Katika Tofauti Zetu: Kujenga Ujirani Mwema**



Waefeso 4:3

“... hifadhi umoja uletwao na  
Roho kwa kuzingatia amani iliyo kati yenu...”

**KAMPENI YA KWRESIMA  
2022**



**CJPD**



C<sup>†</sup>JPD

© KCCB-Catholic Justice and Peace Department, 2022

Ubunifu na utayarishaji:

**Makao Makuu ya Baraza la Maaskofu Wakatoliki Kenya**

**Idara ya Kikatoliki ya Haki na Amani**

Wahariri: **Beatrice Odera, Angela Obadha and Wainainah Kiganya**

Mchoraji: **Robert Kambo**

Msanifu na mpambaji wa kurasa: **Kelvin Malombe**

Mratibu wa michango: **Margaret Mkavita**

Kimepigwa chapa na: **Don Bosco Printing Press,**

**S.L.P. 158 Makuyu 01020, Kenya**

**UMOJA KATIKA  
TOFAUTI ZETU:  
KUJENGA UJIRANI  
MWEMA**

KAMPENI YA KWARESIMA 2022

# **YALIYOMO**

5	<b>SALA KWA DUNIA YETU</b>
6	<b>DIBAJI</b>
9	<b>UTANGULIZI</b>
10	<b>UFAFANUZI</b>
13	<b>WIKI YA KWANZA: WAJIBU LA KIRIAIA</b>
13	TAZAMA: SIMULIZI
13	AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
14	TAFAKARI YA KIROHO
16	TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
16	KUJICHUNGUZA
16	MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
18	<b>WIKI YA PILI: WOTE KUHESHIMU UTAWALA WA SHERIA</b>
18	TAZAMA: SIMULIZI
18	AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
20	TAFAKARI YA KIROHO
21	TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
21	KUJICHUNGUZA
21	MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
23	<b>WIKI YA TATU: ULANGUZI WA BINADAMU</b>
23	TAZAMA: SIMULIZI
23	AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
25	TAFAKARI YA KIROHO
26	TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
26	KUJICHUNGUZA
27	MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
29	<b>WIKI YA NNE: KUJITOSHELEZA KWA CHAKULA</b>
29	TAZAMA: SIMULIZI
30	AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
31	TAFAKARI YA KIROHO
33	TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
33	KUJICHUNGUZA
33	MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
35	<b>WIKI YA TANO: VIJANA NA UCHAGUZI WA AMANI</b>
35	TAZAMA: SIMULIZI
36	AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
36	TAFAKARI YA KIROHO
37	TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
37	KUJICHUNGUZA
37	MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
38	<b>MICHANGO YA KAMPENI YA KWARESIMA YA 2021 (KSHS)</b>
73	<b>SALA KWA KADINALI OTUNGA</b>
74	<b>SALA KWA KAMPENI YA KUPAMBANA NA UFISADI</b>

## SALA KWA DUNIA YETU

**E** Mungu Muumba mwenye nguvu zote, uliye ndani ya vitu vyote ulimwenguni ikiwa ni pamoja na viumbe vyako vile vidogo zaidi

Huruma zako zinakumbatia vyote vinavyoishi na vilivyo hai.  
Tunyunyuzie uwezo wa upendo wako,  
ili tuweze kulinda maisha na umaridadi wake.

Tujaze amani yako, ili tuishi kama ndugu wa kiume na wa kike, bila kumdhuru yeyote.

E Mungu mfadhili wa maskini, tusaidie kuwaokoa waliotelekezwa na kusahaulika katika dunia hii,  
wenye thamani kubwa machoni mwako.

Tupe uponyaji maishani mwetu,  
ili tuitunze dunia na wala tusiiharibu,  
kwamba tuvune umaridadi,  
wala sio uchafuzi na uharibifu.

Gusa nyoyo za wale ambao hutafuta kufaidika wenyewe pekee  
bila kuwajali maskini wa dunia.

Tufundishe kuvumbua thamani ya kila kitu,  
tujazwe heshima na kutafakari,  
kutambua kwamba tumeunganika pakubwa  
na kila kiumbe tunaposafiri kuelekea kwenye mwangaza  
wako usio na mwisho.

Tunakushukuru kwa kuwa nasi kila siku.

Tupe moyo, tunakuomba, katika harakati zetu,  
za kutafuta haki, upendo na amani.

*Sala hii ilichapishwa katika waraka wa kitume wa Baba Mtakatifu Francis, Laudato Si'. Ni sala ya wote wanaomwamini Mungu Muumba mwenye nguvu zote.*

### UMOJA KATIKA TOFAUTI ZETU: KUJENGA UJIRANI MWEMA

**W**atu wa Mungu, uchaguzi mkuu wa 2022 unakaribia. Hali ya wasiwasi ambayo ni ya kawaida kila mara uchaguzi unapobisha isipokabiliwa kikamilifu ipasavyo, ni hatari kwa umoja na mshikamano wa taifa letu.

Hatufai kamwe kusahau tulikotoka. Mnamo siku zilizopita, tumepoteza maisha ya wengi, wakiwemo watoto. Watu wamefukuzwa kutoka makwao, wengine wakapata majeraha yaliyowafanya vilema na kupatwa na magonjwa ya akili, hasa mnamo 2007/8 kufuatia kutangazwa kwa matokeo yaliyozozaniwa ya kura ya urais. Na hata uchaguzi uliofuata wa 2013 na 2017 ulikuwa na changamoto zake. Kumbukumbu za matukio hayo zinaumiza nyoyo na fikra na hatuna budi kuazimia kujikinga kutokana na kundi lolote au mtu binafsi mwenye nia ya kuvuruga amani yetu.

Uchaguzi hufanyika na kumalizika. Lakini kuna dosari za shughuli hizo za awali ambazo tunapaswa kuzika na kuhakikisha haziathiri kura zijazo. Maisha yetu hayafai kamwe kuvurugwa na shughuli zo zote, hata ziwe muhimu kiasi gani. Ndiposa tunaangazia kwa njia ya kipekee jinsi uchaguzi mkuu wa mwaka huu utafanyika. Tukishirikana na maaskofu wetu katika mradi wao wa amani, sote tunapaswa kuungana kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani, bila kujali washindi ni nani kuanzia ngazi ya wajumbe wa kaunti hadi urais.

Tutaangazia suala la **Wajibu wa Kiraia** katika **Wiki ya Kwanza**. Hili ni jambo ambalo linahusu matendo na mwelekeo wetu katika jinsi utawala wa kidemokrasia unavyoendeshwa na vile tunashiriki kama jamii katika shughuli za maendeleo za Serikali, Kanisa na jamii kwa jumla kwa lengo la kuimarisha hali ya wananchi.

Tunatekeleza hayo kwa kuelimisha watu wetu waliotimiza umri wa kupiga kura kuhusu haki za kiraia na upigaji kura. Elimu hiyo inawalenga pia maajenti ambao wana jukumu la kuhakikisha haki na amani zinadumishwa wakati wa shughuli za kampeni, siku ya upigaji kura na baada ya matokeo kutangazwa.

Katika **Wiki ya pili**, tutaliangazia suala la **Wote kuheshimu utawala wa sheria** ambalo ni msingi wa kufikia huduma za umma, kupigana na ujisadi na kuimarisha usawa na haki katika ugawaji wa rasilmali nchini. Ni mojawapo ya vigezo vya kuamua kiwango cha hali ya nchi na utawala wake.

Ulanguzi wa binadamu ni tabia ya kishenzi iliyopitwa na wakati. Miaka mingi iliyopita, kuuza watu utumwani kulikubalika kuwa biashara halali. Lakini yasikitisha kukuta kwamba shughuli hiyo ya kinyama inazidi kuimarika katika nchi yetu. Vijana wa kiume na wa kike wanasafrishwa kutoka nchini na kupelekwa mbali kufanya kazi lakini wanaishia kuwa watumwa. Tukiwa Wakristo, tunao uwezo wa kushirikiana na serikali, na mashirika yanayopinga watu wetu kuuzwa utumwani kwa lengo la kuhakikisha vijana wetu hawanaswi na mtego wa magendo hayo. **Ulanguzi wa binadamu**, mada yetu ya mjadala wa **Wiki ya tatu**, ni jambo linalomgusa kila mmoja wetu, awe maskini au tajiri.

**Wiki ya nne** tutashughulikia mada nyingine mbili ambazo ni muhimu kwa Kanisa. Ni jambo linaloleta aibu kukuta kwamba katika karne ya 21, bado kuna watu nchini Kenya ambao hawawezi kupata angalao sahani moja ya chakula kwa siku. **Kujitosheleza kwa chakula** katika nchi yetu ni jambo linaloweza kufanikishwa. Mungu ametubarikia ardhi yenye rutuba, wananchi wenye bidii na ari ya kazi na mazingira yafaayo kwa uzalishaji wa chakula cha kumlisha kila mtu. Lakini kwa bahati mbaya, tunayo changamoto; tumemaliza misitu kwa ukataji ovyo na haramu wa miti, tumejenga kando kando ya mito na kuimarisha shughuli zetu mbali mbali kwenye ardhi ambazo zinfaa kuhifadhiwa ili kutupatia hewa safi na hasa katika maeneo ya miji. Baba Mtakatifu Francis, kwenye waraka wake wa kitume *Laudato Si*, anatuhimiza kukumbuka kwamba ni jukumu letu kumtuza mama wetu ardhi. Mabadiliko ya hali ya anga ni halisi. Tunapaswa kushirikiana kuhahakiksha hatuyaharibu maumbile ambayo hatimaye yatatuumiza. Inawezekana kutafuta mbinu za kuyafufua mazingira na kuyajenga upya kwa manufaa yetu na ya vizazi vijavyo.

Katika **Wiki ya tano** tutatilia mkazo umuhimu wa kuhakikisha vijana wetu hawatumiwi vibaya na wanasiasa na kufuata kiholela porojo za kisiasa kama inavyoelezwa kwenye mjadala wa **Vijana na uchaguzi wa amani**. Tumeshuhudia jinsi wanaowania nyadhifa za kisiasa wamewatumia vijana kuhusika na matendo maovu kama

vile kuwakashifu wapinzani wa wadhamini wao, kuwashambulia wanaoshukiwa kuwa maadui na hata kuwadhuru watu wasio na hatia.

Vijana wetu wanapaswa kuwa nguzo muhimu katika mradi wetu wa elimu ya haki za uraia na upigaji kura. Wana uwezo na nguvu za kuhimiza kudumishwa kwa amani mionganoni mwa wanasiasa wa milengo tofauti na mawazo yanayopingana.

Ni wajibu wetu tukiwa Kanisa kuhakikisha kwamba vijana wanatimiza jukumu la kuinufaisha jamii wakiwa raia ambao wana uwezo wa kuamua jisni maisha yao ya siku zijazo yatakuwa.

Tunawaalika nyote kuutumia msimu huu wa Kwaresima kuombea amani na uelewano katika nchi yetu na kushiriki katika matendo ambayo yatatuhakikishia umoja wa taifa na kuimarisha ujirani mwema.

Nawatakieni nyote, enyi wapendwa watu wa Mungu, msimu wa Kwaresima uliojazwa Roho wa Mungu na wenye mafao.

*Askofu John Owaa Oballa wa Jimbo la Ngong'*

*Mwenyekiti, KCCB-CPIHD-Idara ya Kikatoliki ya Haki na Amani*

## UTANGULIZI

### Kwaresima katika Kanisa Katoliki

**K**waresima ni kipindi cha siku 40 cha kufunga na kujinyima, kusali na kutubu kabla ya Pasaka. Kulingana na utamaduni wa Kikristo, msimu huu katika mwaka wa kiliturjia huanza Jumatano ya Majivu na kumalizika Jumapili ya Matawi. Ni adhimisho la kila mwaka ambalo huwatayarisha waumini – kupitia sala, toba, kutoa zaka na kujinyima – kwa matukio yanayohusiana na mateso ya Yesu msalabani, na maadhimisho ya ufufuko wake. Wakatukumeni hubatizwa Jumapili ya Pasaka.

### Kwa nini siku 40?

**N**ambari 40 ni muhimu katika maisha ya Wakristo. Musa na wana wa Israeli, kwa mfano, walitanga jangwani kwa miaka 40 wakijandaa kwenda katika nchi waliyoahidiwa na Mungu. Musa alikaa juu ya Mlima Sinai kwa siku 40 bila kula wala kunywa alipokuwa ameenda kupokea vibao vyya mkataba ambao Mungu aliwawekea Waisraeli. Nyakati za Nuhu, gharika iliendelea kwa siku 40 mchana na usiku. Eliya alikaa siku 40 mchana na usiku juu ya Mlima Horebu bila chakula. Yesu naye alienda jangwani na kufunga kula na kunywa kwa siku 40 mchana na usiku.

### Asili ya Kampeni ya Kwaresima Kenya

**K**uzingatia wito wa kiroho wa msimu wa Kwaresima, Kanisa Katoliki katika Kenya liliazimia kuwapasha waumini habari kuhusu matatizo yanayokumba jamii na kushirikiana nao kutetea mabadiliko. Kupitia kwa Kampeni ya Kwaresima, Maaskofu wa Kanisa Katoliki huwaita Wakristo wote na watu wa mapenzi mema kuungana na kukabiliana na matatizo hayo, huku wakiteteta mabadiliko. Kwa kuungana na maaskofu katika utetezi huo wa mageuzi, juhudzi za kila mtu binafsi pamoja na sauti ndogo ya kila mmoja ikiunganishwa na ya wengine husikika mbali, nayo matendo ya kila mmoja huongezeka yakijumuishwa na ya wengine.

## MAFUNDISHO YA KANISA KATOLIKI KUHUSU JAMII

**M**afundisho ya Kanisa Kuhusu Jamii ni mashauri ya thamani na ya busara kuhusu jinsi ya kujenga jamii yenye haki na inayozingatia maisha matakatifu bila kujali changamoto za jamii ya kisasa. Mafundisho haya yamekuwa yakinolewa kupitia kwa nyaraka za kitume za Baba Mtakatifu, daftari za Vatican Council II na taarifa za mabaraza ya maaskofu ambazo mada zake kuu ni:

### **Maisha na hadhi ya binadamu**

Kanisa Katoliki hutangaza kwamba maisha ya binadamu ni matakatifu na hadhi ya mtu ndiyo msingi wa maadili na unyoofu wa jamii. Imani hii ndiyo msingi wa kanuni zote za mafundisho yetu kuhusu jamii. Katika jamii yetu, maisha ya binadamu yametishiwa na utoaji wa mimba na vifo vya huruma. Thamani ya maisha ya binadamu inatishiwa na mtindo wa kupata viumbwe kutoka kwa kiumbe kimoja bila kuunganisha mbegu za kiume na mayai ya kike, utafiti wa seli za viinitete, na adhabu ya kifo. Ni makosa kuwalenga makusudi raia wakati wa vita au kwa mashambulizi ya kigaidi. Mafundisho ya Kanisa yanatuhimiza pia kujitahidi kuepuka vita. Ni lazima mataifa yalinde haki ya uhai kwa kutafuta mbinu thabiti za kuzuia na kusuluhiha migogoro kwa amani. Tunaamini kwamba kila binadamu ana thamani kubwa, watu ni muhimu zaidi kuliko mali, na kipimo cha kila jamii ni iwapo inatishia au inaimarisha maisha na hadhi ya mwanadamu.

### **Wito kwa familia, jamii na ushiriki**

Binadamu sio tu mtakatifu lakini pia anaishi katika jamii. Mpangilio wa jamii kiuchumi, kisiasa, kisheria na sera hugusa hadhi ya kila mtu na kuathiri uwezo wa watu binafsi kukua katika jamii. Ndoa na familia ni nguzo kuu za jamii na ni lazima ziungwe mkono na ziimashwe, wala sio kudunishwa. Tunaamini watu wana haki ya kushiriki katika jamii, na kushirikiana kwa manufaa ya wote, na hasa maskini na wasio salama.

### **Haki na wajibu**

Utamaduni wa Kikatoliki hutufundisha kuwa hadhi ya binadamu inaweza kulindwa, nayo jamii imara hupatikana tu iwapo haki za

binadamu zitahifadhiwa na majukumu kutekelezwa. Ndiposa kila binadamu ana haki ya kimsingi ya uhai na vyote anavyohitaji kwa maisha ya heshima. Kwa upande mwingine tunayo majukumu na wajibu kwa wengine, familia na jamii yote.

### **Haki ya kuwajali maskini na wasio salama**

Mtihani wa kimsingi wa mwelekeo wetu kimaadili ni hali ya wasio salama na wanaojipata katika tishio la kuumizwa. Kwenye jamii inayokumbwa na migawanyiko mikubwa kati ya matajiri na maskini, utamaduni wetu unatukumbusha simulizi kuhusu Hukumu ya Mwisho (Mathayo 25:31-46) na kutuamuru kuyapatia kipaumbele mahitaji ya maskini na wasio salama.

### **Hadhi ya kazi na haki za wafanya kazi**

Ni lazima uchumi uwahudumie watu, wala sio watu kutumikia uchumi. Kazi sio tu mbinu ya kujipatia riziki maishani; ni njia ya kuendelea kushirikiana kuchunga yote yaliyoumbwa na Mungu. Ili kulinda hadhi ya kazi, haki za kimsingi za wafanya kazi wote ni lazima ziheshimiwe, nazo ni pamoja na haki ya kazi yenye tija, mishahara ifaaayo na ya haki, kulindwa kwa mali binafsi na juhudzi za kiuchumi.

### **Umoja na mshikamano**

Sote tu familia moja ya wanadamu, bila kujali uraia, rangi, hali ya kiuchumi na tofauti za kimawazo. Sisi ni waangalizi wa ndugu zetu wa kiume na kike popote walipo. Kupenda majirani ni tendo lenye mwelekeo wa kimataifa katika ulimwengu wetu unaozidi kuwa mdogo. Kiini cha tendo adilifu la umoja na mshikamano ni kuzingatia haki na amani. Baba Mtakatifu Paulo VI alitufundisha kwamba ukitaka amani, fanya bidii kutenda haki. Injili inatusihi tuwe waleta amani. Ili kuonyesha upendo kwa ndugu zetu wa kiume na kike, na lazima tuimarishe amani katika dunia yetu iliyooja migogoro na fujo.

### **Kutunza vyote vilivyoumbwa na Mungu**

Tunaonyesha heshima kwa Muumba wetu kwa jinsi tunasimamia vitu vyote alivyoviumba. Kuitunza ardhi ni kanuni muhimu ya imani yetu. Tunatakiwa kulinda watu na dunia, kwa kuishi tukitunza imani yetu kwa kuheshimu vyote vilivyoumbwa na Mungu. Changamoto hii ya kimazingira ina mwelekeo muhimu wa kimaadili ambao hauwezi kupuuziliwa mbali.

wachache wajifokeza kuchukuka kura

jiamatikishe

kura wapijaji

kura wa kapa

wapijaji kura wachache

Sjali!



wa Mapato


SKU YA ELIMU YA  
JAMII YA MAPATO



Mradi wa Maji wa  
Jamii ya Mapato

SHULE YA  
MAPATO

HOSPITAL



# WIKI YA KWANZA WAJIBU WA KIRAI

## TAZAMA: SIMULIZI

**W**anakijiji wa Mapato wakiwachagua viongozi wao, walitilia mkazo tabia, heshima na maadili ya kila aliyekuwa akitafuta uongozi. Walijitahidi kudumisha sifa hizo kwa kujiheshimu kibinagsi na kama mizani ya kuchuja wote waliotamani kuwaongoza. Walikusanyika kila mara kujadili masuala ya jamii na walifuata kanuni na sheria katika harakati za kuchukua maamuzi. Watoto na vijana walidumisha taratibu hizo kila mahali, iwe ni shulenii au kwenye shughuli za kila siku za maisha. Wote waliishi kwa amani na uelewano.

Mawimbi alirejea nyumbani kutoka ng'ambo baada ya kumaliza masomo. Ingawa alitamani uongozi wa kisiasa, hakufikia kiwango kilichohitajika kijijini. Alikuwa ameathiriwa pakubwa na taratibu za uongozi za kigeni na kuyasahau mengi muhimu kijijini. Uchaguzi ulipokaribia, wanakijiji walianza harakati za kawaida za kumtafuta kiongozi. Mawimbi hakuwa mionganii mwa wagombeaji walioteuliwa. Alipotambua tatizo lake, akaamua kuhonga wafuasi. Hatimaye alichaguliwa, bila kuijali manifesto yake duni.

Chini ya uongozi wa Mawimbi, usimamizi wa rasilmali ulikuwa mbaya na zilitumiwa vibaya. Mikutano ya jamii kujadili miradi iliyopendekezwa na masuala ya jamii haikufanyika tena. Ndiposha wakazi wakagundua kosa lao la kutupilia mbali maadili yao ya thamani na kupuuzilia jukumu la kufanya uteuzi bora. Uchaguzini uliofuatia, mbinu ya Mawimbi ya kutumia pesa akitaraji kununua ufuasi haikumsaidia, kwani hakuchaguliwa tena.

## AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Katiba ya Kenya katika utangulizi, inatambua matarajio ya Wakenya kwa Serikali iliyo na misingi bora ya haki za binadamu, usawa, demokrasia, haki za kijamii na utawala wa kisheria; wakitumia uhuru wao na haki yao ya kuamua aina ya uongozi wanaotaka.

Wajibu wa kiraia unahu su matendo na michango yetu kwa utawala wa kidemokrasia, na ushirika wetu katika shughuli za maendeleo za Serikali, Kanisa na jamii kwa jumla kwa lengo la kuimarisha hali ya wananchi. Tushiriki katika taratibu za kidemokrasia kwa

kuwachagua viongozi au sisi kuchaguliwa ili kuhakikisha uongozi bora unadumishwa. Tunaweza pia kujitolea kuwa wanachama wa mashirika ya jamii, kushiriki katika mijadala ya kitaifa, kuzuia na kupigana na ujisadi na kuimarisha utumiaji bora wa rasilmali.

Kenya inakumbwa na tatizo la watu kujali tu maslahi ya kibinafsi ya kisiasa na kuwafanya wengine njama. Ujisadi umeenea kote katika mashirika ya umma na ya binafsi. Wapigaji kura wengi hawana imani tena kwamba taratibu za kisiasa zina manufaa yoyote kwao. Wameamini kuwa juhudini zozote za kujaribu kuleta mabadiliko ni kazi bure. Hali hiyo huenda imewavunja wengi moyo wa kuyajali majukumu ya kitaifa. Matokeo ya watu binafsi au makundi kukata tamaa ya kupiga kura au kubeba majukumu mengine ya kitaifa ni kuchaguliwa kwa viongozi dhaifu.

Ili kukabiliana na tatizo la wapigaji kura kususia uchaguzi na wananchi kupuuza majukumu yao ya kiraia, kila mmoja wetu anafaa kuzingatia sheria. Kifungu 10 (2) (a) cha Katiba kinalezea maadili ya kanuni za uongozi, nazo ni pamoja na uzalendo, umoja wa kitaifa, kushirikiana, ugatuvi wa mamlaka, utawala wa sheria, demokrasia na kushiriki kwa watu. Kifungu 81 kinatoa kanuni za jumla za mfumo na utaratibu wa uchaguzi. Kifungu 38 kinampa kila raia uhuru wa kuwa na uchaguzi wa kisiasa, na haki ya kuunda, au kushiriki katika uundaji na shughuli za chama cha kisiasa.

Mafunzo ya Kanisa Kuhusu Jamii pia yanatukumbusha na kuhimiza haja ya kutilia maanani jukumu letu la kiraia kwa lengo la kuimarisha manufaa kwa wote, kuheshimu haki isiyofaa kukiukwa ya hadhi ya uhai wa binadamu na kuwajali maskini.

Tukiwa raia wanaowajibika, tunapaswa kujitahidi kutathmini na kuchagua viongozi wafaa na wanaojali kanuni za utumishi kwa wanadamu na kwa usimamizi thabiti wa maumbile na mazingira.

## **TAFAKARI YA KIROHO**

**Kumbukumbu la Sheria 26:4-10**

**Waroma 10:8-13**

**Luka 4:1-13**

Katika Injili ya leo, Yesu anamwambia shetani wazi wazi asithubutu kumjaribu Bwana, Mungu wetu. Mtakatifu Paulo akiwaandikia Wakristo wa Roma anawahimiza kuhusu jinsi wanapswa kuishi maisha matakatifu. Anashauri: "*Msiige mitindo ya ulimwengu huu,*

*bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu na kutambua jambo lililo jema, linalompendeza kikamilifu” (Waroma 12:2).*

Kwaresima ni kipindi cha kukarabati mawazo yetu na kutambua mapenzi ya Mungu kwa kuweka nidhamu ya kiroho ya kutuwezesha tusiige mitindo ya ulimwengu. Ili kudumisha hadhi yetu kama raia binafsi na pia kwenye makundi, tuzingatie haki yetu asilia ya kujali masuala ya umma, ambayo ni pamoja na kushiriki kikamilifu katika shughuli za serikali na kutoa michango mahsus kwa manufaa ya wote. Tunapaswa kuwa na uhuru wa kutekeleza wajibu wetu wa kiraia kikamilifu, huku lengo letu likiwa ni manufaa kwa wote.

Haja yetu kuu inapaswa kuwa ni kuelewa kikamilifu mahitaji ya jamii. Kumtii Mungu na kuzingatia viwango vyake ni kuwa makini kufahamu jukumu letu maalumu na kamili katika jamii ya kisiasa. Wakristo wanafaa kuwa mfano dhahiri wa moyo wa uwajibikaji na kujitolea kwao kwa manufaa ya wote.

Raia wanapaswa kuendeleza kwa ukarimu na uaminifu moyo wa uzalendo bila kupuza mawazo ya wengine. Kila mmoja anahitaji kila mara kudumisha maslahi ya wanadamu wote, bila kujali asili, mbari au uraia. Tunahitaji kujenga utamaduni ambapo raia hutamani na kubuni mpango wa pamoja ambao lengo lake si kunufaisha mtu binafsi au kutosheleza tamaa za kibinafsi. Tunahitaji kuchagua viongozi wa kisiasa wanaoweza kushauriana nasi kwa dhati na kikamilifu ili kufikia kina – na sio tu sura – cha maovu ulimwenguni. Wanasiasa wetu wanapaswa kusumbuliwa akili kwa dhati na hali ya jamii, watu na maisha ya maskini.

Watu katika kila taifa wanahitaji kuendeleza hali za kijamii za maisha yao kwa kujitolea na kuwajibika, wala sio kufuata halaiki ambayo huyumbishwa na mashirika na makundi yenye kuzingatia maslahi ya kibinafsi. Uwajibikaji kiraia ni tendo adilifu na kushiriki katika shughuli za kisiasa ni wajibu. Watu binafsi na makundi mashinani wanaweza kuleta mabadiliko kamili. Wanaweza kuhimiza kiwango cha juu cha uwajibikaji, moyo wa kujali jamii, wawe tayari kulinda wengine, wawe na moyo wa kubuni na mapenzi yasiyo na kifani ya ardhi. Huwa wanajali pia urithi kwa watoto na wajukuu wao hatimaye. Jamii, kuitia kwa mashirika yasiyo ya serikali na makundi suluhishi, inapaswa kuishurutisha serikali kubuni sheria, kanuni na taratibu kali zaidi. Raia wasiposimamia mamlaka ya kisiasa katika ngazi za kitaifa, mikoa na kaunti, haitawezekana kudhibiti hasara na madhara hata kwa mazingira.

Sio kila mtu ameitwa kushiriki moja kwa moja katika maisha ya siasa. Jamii pia imebarikiwa kuwa na mashirika tofauti yasiyohesabika yanayofanya kazi kwa lengo la kuimarisha manufaa kwa wote na kulinda mazingira asili na watu wake. Katika shughuli hizi zote za kijamii, mahusiano hujengwa au kufufuliwa na mfumo mpya wa kijamii huibuka.

Hivyo basi, jamii inaweza kujinasua kutoka kwa hali ya kutojali inayosababishwa na ufujaji. Matendo hayo hujenga njia mpya ya kujitambulisha inayoandamana na simulizi liwezalo kukumbukwa na kupashwa wengine. Kwa njia hii, dunia na kiwango cha maisha ya walio maskini zaidi, hutunzwa kwa moyo wa umoja ambao wakati huo huo unatambua tunaishi sote katika makao ya pamoja ambayo Mungu alitukabidhi tutunze.

## **TENDA: MASWALI YA KUWAZIA**



- » Je, unaelewaje wajibu wa kiraia?
- » Je, wajibu wangu kama raia ni upi katika jamii?
- » Je, Kanisa lina jukumu gani katika kuimarisha wajibu wa kiraia?

## **KUJICHUNGUZA**

- » Mimi ni raia anayewajibika kwa njia gani?
- » Ninawezaje kuwa raia anayewajibika?
- » Ninaimarishaje wajibu wa kiraia katika familia yangu, jamii, parokia na jimbo?

## **MATENDO YALIYOPENDEKEZWA**

- » Tafuta elimu ya haki za kiraia na uwaelimishe wengine.
- » Shiriki katika taratibu za uchaguzi ukiwa wajibu wako wa kisheria; pata kitambulisho cha kitaifa, jiandikishe kuwa mpigaji kura, piga kura na uwahimize wengine kufanya vivyo hivyo.
- » Watambue na kuwakataa viongozi wafisadi, na uwapigie kura viongozi waadilifu.
- » Tia sahihi fomu ya kujitolea kuunga mkono kampeni ya kanisa Katoliki kupigana na ujisadi.



AHSANTE KWA  
HUDUMA ZAKO NZURI

# WIKI YA PILI WOTE KUHESHIMU UTAWALA WA SHERIA

## TAZAMA: SIMULIZI

**M**istani alikuwa kiongozi wa Jimbo la Mashaka. Siku moja akiendeshea gari upande usiofaa wa barabara, kama alivyozoea, alimgonga mwendesha baiskeli aliyeitwa Mpole. Alitoroka na kuiacha motokaa yake katika eneo la ajali. Mashahidi walimwokoa Mpole lakini wakavunja madirisha ya gari lililomjeruhi na kutoroka punde tu polisi walipowasili. Mpole alipelekwa hospitali na Wasamaria wema na ikabidi akatwe miguu.

Mmoja wa mashahidi alinasa tukio lote kwa simu na kulisambaza moja kwa moja kupitia kwa mitandao ya kijamii. Picha hizo ziliwakasirisha wengi. Mashirika ya kupigania haki za binadamu na makundi mengine ya watetezi yalitaka Mistani ashtakiwe na wakashutumu walioharibu motokaa yake. Walitaka Mpole atendewe haki. Polisi walianzisha uchunguzi na kuwaalika mashahidi kuandikisha taarifa. Baadhi ya mashahidi waliogopa kujitokeza kwa sababu ya visa vya awali ambapo mashahidi katika kesi zilizohusu watu mashuhuri walitoweka na wasipatikane tena.

Mistani alitiwa nguvuni na kushtakiwa. Lakini kwa sababu ya wadhifa wake kisiasa na kuungwa mkono na viongozi wengine, aliondolewa mashtaka na kuachiliwa huru bila masharti. Vyombo vya habari havikumpa nafasi ya kupumua kwani viliedelea kuiangazia hali ya Mpole. Majeruhi huyo hangeweza kugharamia matibabu yake wala kukimu mahitaji ya familia yake kwa sababu ya majeraha aliyyopata ajalini. Raia walifanya maandamano ya amani wakitetea haki na utawala wa sheria. Wengi walitia sahihi maombi ya mitandao ya jamii kuhimiza Mistani kufutwa kazi. Hatimaye Mistani aliachishwa kazi na miezi mitatu baadaye, haki ilitekelezwa wakati Mpole alilipwa fidia na Mistani akahukumiwa.

## AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Utawala wa sheria ni msingi wa kufikia huduma za umma, kupigana na ujisadi na kuimarisha usawa na haki kwenye ugawajji wa rasilmali katika maeneo yetu mbali mbali. Ni mojawapo ya vigezo vya kuamua kiwango cha hali ya nchi na utawala wake. Utawala wa kisheria unawapasa wote wenye mamlaka kuyatumia

kulingana na mipaka ya sheria na kuzingatia kanuni za umma zilizowekwa, wala sio kufanya mambo kiholela au kwa hiari yao au kuzingatia hali ya mawazo yao. Utawala wa sheria huitaka Serikali kuendesha shughuli zake kisheria na kuwajibika ipasavyo kila mara walio mamlakani wanapotenda kinyume. Raia nao wanapaswa kuheshimu na kuzingatia kanuni zote halali, hata kama hawakubaliani nazo.

Umoja wa Mataifa husisitiza kwamba utawala wa sheria unapaswa kuleta matokeo yanayotarajiwa na ya kufaa katika utendaji na matumizi kwa lengo la kujenga amani ya kimataifa, usalama na utulivu wa kisiasa. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu unakariri kwenye utangulizi wake hadhi asili na haki sawa kwa wanadamu wote zikiwa msingi wa uhuru, haki na amani ulimwenguni (UNDHR, 1948).

Mkataba wa Kiafrika wa Haki za Binadamu na Watu (ujulikanao pia kama Mkataba wa Banjul) unasisitiza umuhimu wa kuzingatia, kuimarisha na kulinda utawala wa sheria barani. Kadhalika, Ajenda 63 ya Muungano wa Afrika inatambua kuwa utekelezaji na ufanikishaji wake utabainishwa na serikali na taratibu ambazo huzingatia kikamilifu utawala wa sheria kulingana na kanuni bora zaidi za kimataifa.

Katiba inathibitisha mamlaka yote makuu ni ya wananchi wa Kenya na yanaweza kutekelezwa tu kulingana na sheria hii kuu. Hili linatekelezwa kupitia kwa kanuni zenyelengo la:

- » Kuimarisha na kulinda taifa kuzingatia misingi ya umoja wa taifa na uaminifu wa kisiasa, huku tukiheshimu tofauti zetu za kikabilu, kitamaduni na kidini;
- » Kuimarisha demokrasia na kugawa mamlaka ya Serikali;
- » Serikali ya kitaifa na za kaunti ni tofauti na zinategemeana;
- » Kulinda maadili na kanuni za uongozi katika utumishi wa umma;
- » Kuanzisha na kuimarisha mashirika huru na ya kikatiba ili kuhudumia Wakenya wala sio kuwafanya watumwa; na
- » Kuyapatia maadili kipaumbele katika utawala wa umma kwa manufaa ya wote.

Kila mtu ni sawa mbele ya sheria na ana haki ya kulindwa na kupata manufaa sawa ya sheria. Sheria inafaa kufikiwa kwa urahisi; taasisi za kisheria na kanuni zake zinapaswa kupatikana kwa urahisi na raia wa kawaida kwa lengo la kudumisha haki zao, kusuluhisha mizozo yao na kuwalinda kutokana na matumizi mabaya ya mamlaka ya umma au ya binafsi.

Matokeo ya kutotunza au kutoijua sheria ni dhuluma. Mafundisho ya Kanisa Kuhusu Jamii huthibitisha haja ya sheria katika jamii ili kulinda raia, kudumisha taratibu na kuwawezesha kuishi kwa amani. Manufaa kwa wote yanahitaji wote walio na mamlaka kwa raia wawe waangalifu na kudumisha usawa katika kusimamia, kulinda na kuimarisha haki za raia. Shughuli za serikali zinapaswa kupanua uhuru kadiri iwezekanavyo kwa kulinda kikamilifu haki muhimu za kila mtu binafsi.

## **TAFAKARI YA KIROHO**

**Mwanzo 15:5-12.17-18**

**Wafilipi 3:17- 4:1 or 3:20- 4:1**

**Luka 9:28b-36**

Injili ya leo inaturalika kumsikiliza Yesu akitueleza kwamba sheria ni kwa manufaa ya wanadamu. Lengo lake ni kuhakikisha kwamba haki na hadhi za binadamu zinalindwa. Tunahimizwa kuheshimu utawala wa sheria.

Walinda sheria ni lazima waizingatie nyakati zote huku wakiheshimu haki za binadamu na hadhi. Maafisa wa umma wanahimizwa kudumisha utaalamu na utu, maarifa na busara bila kuvunjika moyo wala kukata tamaa. Watumishi hao watambue kwamba maisha ya wanaume na wanawake wengi — pamoja na matatizo na matarajio yao — hutegemea matendo na maamuzi ya watumishi hao.

Wahudumu wanapaswa kuzingatia sheria kwa kutekeleza kwa usahihi kanuni na masharti ya kisheria yanayohakikisha heshima kwa haki za msingi za kila binadamu. Wanafaa kuongozwa na dira ya mfumo usioweza kuondolewa wa kutii sheria, kujali mahitaji ya binadamu na kuwa na imani na mashirika ya umma.

Utamaduni unaoendelea kumea mizizi wa kupuuza sheria na kutojali kuadhibiwa unatia hofu. Baadhi ya watu binafsi wenye mamlaka, hasa wanasiasa, ambao hujiona wako juu ya sheria na huvunja sheria na kutoa matamshi yasiyofaa bila kujali kuadhibiwa. Mazoea haya yanafaa kuzimwa ili tudumishe utawala wa sheria.

Lakini tuna tatizo kubwa katika nyanja za umma na binafsi na madhara yake ni makubwa, hasa katika elimu. Matokeo yake ni kuongezeka kwa visa vya mazoea ya kutotii mamlaka, kutotaka kuwasikiliza wengine na kutokuwa na subira.

Shabaha ya kutekeleza mamlaka ni kufikia manufaa kwa wote na hali hiyo hubainika wakati mamlaka yanafahamika kama huduma, sawa na alivyofanya Yesu Kristo ambaye alikuja kuhudumu wala sio kuhudumiwa.

Kadiri raia wanavyothibitisha kwamba shabaha ya mamlaka ni kujaribu kuleta suluhu, kutoa majibu kwa mahitaji yao na kulinda haki zao, ndivyo watakuwa tayari kuzingatia maagizo, kuwa makini na kupata moyo wa kushirikiana na kuonyesha heshima.

## **TENDA: MASWALI YA KUWAZIA**


- » Je, unauelewa vipi utawala wa sheria?
- » Utawala wa sheria hutekelezwaje katika nchi yetu?
- » Tuna jukumu gani kudumisha na kuheshimu utawala wa sheria?
- » Tunazingatiaje sheria za makundi yetu tofauti (chama, jumuia, parokia na jimbo)?

## **KUJICHUNGUZA**

- » Ninauheshimu utawala wa sheria?
- » Nimemshawishi ye yeyote kutoheshimu utawala wa sheria?
- » Nimekuwa mtetezi wa utawala wa sheria?

## **MATENDO YALIYOPENDEKEZWA**

- » Toa sauti wakati viongozi na raia wanapokataa kuheshimu utawala wa sheria.
- » Jadili jinsi ya kuheshimu na kudumisha utawala wa sheria katika ngazi ya jamii.
- » Andaa mikutano inayoshirikisha sekta tofauti katika ngazi za kitaifa, kaunti na jamii kusisitiza haja ya kuheshimu utawala wa sheria.
- » Tia sahihi na uweke ahadi ya kuunga mkono kampeni ya Kanisa Katoliki kupigana na ufisadi.



MP RANGO  
AGENCY

HAYA HARA  
MALIPO YAKO

AREANTE,  
UMEMALIZA  
KWAWAKATI  
UFALAO

NEAMBO

# WIKI YA TATU ULANGUZI WA BINADAMU

## TAZAMA: SIMULIZI

**K**ijiji cha Kwenu kilijaa wanaume na wanawake mashuhuri. Mila na tamaduni zake zilizingatia kiwango cha juu cha maadili. Wanakijiji walijihuisha na kilimo na biashara ndogo, ikiwa ni pamoa na biashara ya kubadilishana bidhaa. Walizoea kusaidiana na ilikuwa ni rahisi kumtambua mgeni mionganoni mwao. Maisha yao yalivutia watu wa jamii majirani waliohamia humo, wakaoana na kuwa sehemu ya jamii ya Kwenu.

Kadiri jamii ilivyozidi kuongezeka ndivyo rasilmali ziliendelea kuwa haba na kuwaacha wengi kung'ang'ana kutosheleza mahitaji muhimu. Haja ya kutafuta mbinu mbadala za kujikimu ikaibuka. Mpango, mkazi aliyehamia Kwenu, alianzisha kampuni ya kuwatafutia wanakijiji nafasi za kazi ng'ambo. Waliokuwa wakitafuta ajira na waliohitaji wafanya kazi walimlipa ada za juu alizotoza. Mahitaji makubwa ya wafanya kazi yalimsukuma Mpango kuwasajili wavulana na wasichana wadogo na kuwapelekeea wateja ambaao hakuwa na maelezo ya kutosha kuwalhusu.

Mfansi, mtaalamu wa kusuka nywele na urembeshaji, ni mionganoni mwa waliochaguliwa kwenda ng'ambo kufanya kazi. Alifurahishwa na nafasi hiyo akiamini ingempatia mshahara mkubwa na kuinua kiwango cha maisha. Aliuza biashara yake na mara tu alipowasili ng'ambo, kitambulisho chake, hati za usafiri na simu zilitwaliwa na waajiri wake. Alilazimika kufanya kazi tofauti na ngumu kwa saa nyingi kila siku bila kupumzika wala kupata malipo aliyoahidiwa. Akiugua, hakuruhusiwa kupata matibabu. Alijipata hoi na kujuta kupata hasara ng'ambo na kupoteza mali nyumbani.

Viongozi wa nyumbani walipopata habari za kusikitisha kuhusu Mfansi na wanakijiji wengine waliokwenda ng'ambo, waliamua kuwaelimisha wanakijiji kuhusu masaibu ya wenzao ugenini.

## AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Ulanguzi wa binadamu ni utumwa wa kisasa. Wanaume na wanawake wameendelea kushawishiwa kwa ahadi za uongo za maisha bora ugenini, huku watoto nao wakiendelea kutoroshwa hata na baadhi ya watu wanaowafahamu. Ripoti iliyoolewa na

Kenya mnamo 2020 kuhusu njia zitumiwazo na walangazi wa binadamu inathibitisha kwamba ovu hilo limeenea nchini, na walangazi wenge ari na bidii wanatumia kila mbinu kutambua njia mpya za usafirishaji na kuwanasa ‘wateja’ zaidi.

Ulangazi wa binadamu nchini Kenya umeendelea kuenea kutokana na ongezeko la umaskini, uhaba wa nafasi za kazi na mahitaji ya watu binafsi na ya familia zao. Ndiposa wengi wanatafuta kazi katika nchi za Uarabuni, hasa Saudi Arabia. Wengine husafiri hadi Italia, Uingereza, India, Malaysia na Marekani kuititia kwa maajenti halali na haramu ya uajiri. Kuna wengine ambao huhamia maeneo tofauti ya nchi.

Ripoti moja iliyotolewa na Wizara ya Mashauri ya Kigeni ya Marekani mnamo 2020 imeiorodhesha Kenya kuwa chanzo, njia na nchi inayopokea wanaume, wanawake na watoto wanafanyizwa kazi ya lazima, wanaingizwa utumwani nyumbani na kudhulumiwa kimpenzi. Mara nyingine wanatumiwa vibaya katika vyumba vya huduma za kukanda misili na madanguro au kulazimishwa kufanya kazi ngumu ambazo hazihitaji utaalamu wowote.

Mojawapo ya athari za COVID-19 nchini Kenya ni hatari ya ongezeko la ulangazi wa watu katika hali ambapo umaskini umechacha, ukosefu wa kazi unazidi na visa vya ujisadi mionganoni mwa maafisa wa umma na wa mashirika binafsi vinaongezeka, bila kujali hatua zilizochukuliwa kukabiliana na matatizo hayo. Sababu nyingine ni kutojua, tamaa ya pesa, utekelezaji mbaya wa sheria, mipaka yenye njia nyingi haramu na wakazi wa nchi zilizoendelea kuhitaji pakubwa wafanya kazi wasiojali mishahara ya chini. Kenya ilipitisha sheria ya kukabiliana na ulangazi wa binadamu ya 2010 iliyopiga marufuku ovu hilo na kuimarisha ushirika wa jamii katika vita hiyo. Serikali nyingi zinazingatia mpango wa kitaifa wa kuzuia, kukinga na kushtaki ili kukabiliana na ulangazi wa binadamu.

Akihutubia manusura wa ulangazi wa binadamu katika sherehe ya saba ya siku ya kimataifa ya kuomba na kuakisia juhudhi za kupinga ulangazi wa binadamu mnamo Februari 2021, Baba Mtakatifu Francis alisisitiza kuwa uchumi usio na ulangazi wa binadamu unazo sheria za masoko zinazoimarisha haki wala sio kwa manufaa maalumu ya kibinagsi.

“Ninaongea nanyi nyote mnaopinga ulangazi wa binadamu na walioungana kiroho siku hii ya sala duniani, ambayo pia ina lengo maalumu: *Uchumi bila Ulangazi wa Binadamu*,” akasema

Baba Mtakatifu. Akikumbusha kwamba Februari 8 ni siku ya makumbusho ya kiliturjia ya Mtakatifu Josephine Bakhita – msichana mtumwa aliyetangazwa mtakatifu na aliye ishara kote ulimwenguni ya kujitolea kwa Kanisa kupinga utumwa. Kadhalika, Baba Mtakatifu aliwahimiza “watu wote wenye heri jema wafanye sala, washiriki, wasome na kutafakari kuhusu kupiliana na ulangazi wa binadamu, hasa waliokumbana na ulangazi maishani.”

Mara nyingi waathiriwa hurudi nyumbani maisha ugenini yakiwa magumu na yenye dhiki na mateso yasiyoelezeka. Biashara hiyo ni ya kinyama na ni kinyume na Mafundisho ya Kanisa Katoliki Kuhusu Jamii. Sote tunapaswa kushirikiana kukomesha ovu hilo.

## **TAFAKARI YA KIROHO**

**Kutoka 3:1-8a.13-15**

**1 Wakorintho 10:1-6.10-12**

**Luka 13:1-9**

Somo la kwanza linatuonyesha kuwa Mungu hawezi kukubali watu wake kubaki utumwani. Yeye husikia kilio chao na kumtuma Musa kuwakomboa. Ulangazi wa binadamu ndio utumwa wa nyakati zetu. Ulimwengu ukibaki kutazama huku ulangazi wa binadamu ukiendelea, Kristo anawazungumzia wote wanaohusika na kuwatenga, kuwakataa na kuwadhuru watu wengine kupitia kwa biashara hiyo ambayo ni haramu. Kristo anawazungumzia viongozi katika jamii, wawe ni wa kidini, kiuchumi au kisiasa, akitumia maneno makali kama “wanafiki, pango la wezi, kizazi cha nyoka”, na matamshi mengine kuonyesha kutoridhika kwake. Anawakumbusha pia kuhusu hatari ya kupuuza jukumu la kuwalinda wengine. Wote wanaohusika na ulangazi wa binadamu ulimwenguni wanapaswa kuisikiliza sauti ya Kristo kwa unyenyekevu.

Wanaohusika na biashara haramu na yenye mapato makubwa ya ulangazi na ukahaba wanahitaji kuona aibu na kutambua madhara ya biashara yao. Wanaowanajisi na kuwatumia vibaya wanawake na hata kuwakandamiza katika madanguro na masoko ya ukahaba wanahitaji kuomba kuhurumiwa. Ulangazi wa binadamu kwa shabaha ya kuwatumia vibaya katika ngono ni kinyume na alivyokusudia Mungu alipotuumba kwa mfano wake. Tamaduni zinazokubali ukahaba kuwa shughuli ya kawaida kwa jamii

zinahusishwa pia na ovu na kupanuliwa kwa masoko ya walangazi.

Wakati umewadnia kwa makanisa kutilia maanani hatua nyingi zinazoweza kuchukuliwa kukomesha ulangazi katika mataifa unakoanzia, masoko na maeneo yatumiwayo kwa usafirishaji haramu, na kutafuta mbinu za kuwakomboa waathirika. Yajaribu kuvumbua mbinu za kurejesha hadhi, usawa na kudumisha haki za kila mwanadamu katika ngazi zake na mashirika.

Mjadala huu unaweza kusababisha mabadiliko makubwa hata makanisani. Walangazi na wateja wao wanaowanunua wanawake na watoto kwa lengo la kujistarehesha kimwili wanastahili adhabu huku nao waliouzwa wanahitaji maneno ya ukombozi. Dunia inahitaji mwelekeo mpya unaothamini heshima, upendano, mapatano na usawa. Kanisa linahitaji kuwa katika mstari wa mbele kuuvumisha mwelekeo huo. Wakati umewadnia wa kufanya mazungumzo thabiti kukabiliana haraka iwezekanavyo na ovu la ulangazi. Tunaweza kutenga siku katika kalenda yetu ya kiliturjia kuangazia maswala ya ujinsia, mamlaka, dhuluma, ukatili dhidi ya wanawake wanaoshurutishwa kuhusika na ukahaba au kuuzwa utumwani.

Kwa kuchukua hatua katika kila ngazi za kidini, kisiasa, kiuchumi na kijamii, makanisa yanaweza kuleta tofauti kubwa. Ukweli ni kwamba nguvu za mabadiliko hazipotelei kwenye mawimbi ya nyakati, ila huwa zimetulia na kusubiri wasaa muafaka.

## **TENDA: MASWALI YA KUWAZIA**

- » Je, unaelewa maana ya ulangazi wa binadamu na utumwa?
- » Toa baadhi ya sababu za ulangazi wa binadamu na kuingiza watu utumwani?
- » Kuna mambo katika jamii yako ambayo huimarisha utumwa na ulangazi wa binadamu?

## **KUJICHUNGUA**

- » Je, ninaienzi hadhi ya binadamu kwa kiwango cha juu kadiri iwezekanavyo?
- » Je, nimetetea tendo lolote linalohusiana na ulangazi wa binadamu?
- » Je, nimehusika kwa njia yoyote au kuimarisha ulangazi wa wanadamu?

- » Je, ninamfahamu mtu yejote aliyeuzwa ndani na je ya Kenya? Nimechukua hatua gani kukomesha ulanguzi wa binadamu katika jamii yangu?
- » Je, shughuli zangu katika mitandao ya jamii zinaniweka mimi na familia yangu katika hatari ya kuingia mtegoni wa walanguzi wa binadamu?

## **MATENDO YALIYOPENDEKEZWA**

- » Anzisha kampeni ya kupambana na ulanguzi wa binadamu kwa kuandaa mikakati ya kuelimisha jamii ukitumia redio za jamii za Kanisa Katoliki na majukwaa mengine.
- » Anzisha juhudzi za jamii kuwasaidia waathiriwa wa walanguzi wa binadamu.
- » Tambua na upige ripoti kuhusu mashirika laghai ya uajiri.
- » Anzisha miradi ya vijana na watoto kanisani kuhusu uwajibikaji katika utumiaji wa mitandao ya jamii na kulinda watoto.
- » Vumisha utumiaji wa vipawa na maarifa, ubunifu na uzinduzi ili kutoa nafasi za kazi na kuinua kiwango cha maisha.



HAKURA  
CHA  
ISAADA

# WIKI YA NNE KUJITOSHELEZA KWA CHAKULA

## TAZAMA: SIMULIZI

**B**araka aliondoka kutoka kijiji cha Msitu mara tu baada ya kufuzu masomo ya sekondari kwenda kujiunga na Chuo Kikuu cha Kilimo Bora kwa masomo ya digrii ya kilimo na mazingira. Baada ya kuhitimu, aliajiriwa kazi na kampuni kubwa ya ujenzi jijini Maghorofa. Ni kazi iliyokuwa na mshahara mzuri na marupurupu, hasa kwa sababu ya ongezeko la watu waliohitaji nyumba za makazi au kuwekeza katika ujenzi. Baraka na familia yake waliishi jijini na alijivunia mchango wake kwa ustawi wa jiji.

Baada ya muda, janga la maradhi ya kuambukizana lilitokea nchini, likavuruga uchumi, likasababisha wengi kufutwa kazi na kupanda kwa gharama ya maisha. Wengi walishindwa kuyamudu maisha, akiwemo Baraka, baada ya kufutwa kazi. Maisha yalipozidi kuwa magumu, aliamua kurudi kijijini. Alishtushwa na hali ya kuhofisha na kutisha ya kijiji chake ambacho zamani kilivutia.

Badala ya kufunikwa na miti, moshi ulijaa hewani na paa zenye mabati yaliyoingia kutu zilioneekana kote kijijini. Joto lilienea kote, mashamba yalikauka na hayakuwa na mazao yoyote. Wakazi walilazimika kuagiza bidhaa ghali za kilimo kutoka nje. Baraka alipohoji kuhusu ni lini ilinyesha kwa mara ya mwisho, aliarifiwa miaka kadhaa ilishapita. Kijiji kilipokuwa kimefunikwa na kuzingirwa na misitu, ilikuwa ni kawaida kuona malori yakibeba makaa na miti katika iliyoonekana kuwa biashara yenye faida nono kwa baadhi ya wanakijiji binafsi. Wazazi walikatakata mashamba yao vipande vidogo ambavyo havikufaa kwa kilimo na wakawagawia watoto wao. Miti zaidi ilikatwa kutoa nafasi ya kiwanda cha matunda.

Baraka alikumbuka jinsi walikuwa wakipanda kahawa kwenye matuta ya mkingamo na kutumia mbolea kukuza maboga, kiazi kikuu, mihogo, *nduma*, miwa na mimea mingine ya kiasili katika mashamba yaliyojaa unyevu. Mbinu hii ya kilimo ilikuwa na manufaa tele, ikiwa ni pamoja na chakula cha kutosha na salama, hewa na maji safi, miamba ya chumvi kwa wanyama kulamba, madini mengi na watu wenye afya nzuri kwa jumla. Ukame na njaa zilikuwa nadra.

Baraka alitambua umuhimu wa mbinu ya kilimo mseto

iliyoshirikisha mitindo ya zamani na ya kisasa. Hatimaye alipata nafasi ya kutumia yote aliyojifunza chuoni. Alianzisha makundi ya wanawake na vijana ya kujihusisha na kilimo kilichotilia mkazo uhifadhi wa mazingira. Alianzisha pia miradi ya kukinga mazingira. Juhudi hizo zote alizifanya kupitia kwa Kanisa la kijijini na jamii zilisaidia kurejeshea Msitu sifa.

## **AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI**

